TANGAZO LA SERIKALI NA. 362 la tarehe 4/9/2015

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 6 na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA (USHURU WA KUEGESHA MAGARI NA PIKIPIKI) ZA MWAKA, 2015

SEHEMU YA KWANZA:
UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo (Ushuru wa Kuegesha Magari na Pikipiki) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mwaka, 2015 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri

Sura ya 288

3. "Afisa Muidhiniwa'' maana yake ni Afisa aliyeteuliwa kusimamia Sheria hizi.

"Gari" maana yake ni chombo chochote chenye mashine ambacho kinatumia magurudumu manne au zaidi.

'Pikipiki' maana yake ni chombo chochote chenye machine ambacho kinatumia magurudumu mawili au matatu.

"Halmashauri'' maana yake ni mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

"Maegesho" maana yake ni sehemu ya kuegesha gari ambayo italipiwa aidha kwa saa, siku, mwezi au mwaka.

"Mtaa" maana yake ni barabara, njia au eneo la umma ambapo Halmashauri inaweza kuainisha kuwa sehemu ya kuegesha gari.

"Sehemu ya kuegesha pikipiki na gari" maana yake ni sehemu yoyote ile iliyopo katika eneo la Halmashauri ambayo itakuwa imeanishwa kwa mujibu wa Sheria hizi Ndogo kuwa ni sehemu ya kuegesha pikipiki na magari.

"Wakala" Maana yake ni mtu au kampuni yeyote iliyoteuliwa na Halmashauri kusimamia kazi za ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ya magari.

SEHEMU YA PILI
USHURU WA MAEGESHO

.

Sehemu ya Kuegesha

4.-(1) (a) Mitaa yote katikati ya mji ina sehemu za kuegesha pikipiki ama magari kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(b) Halmashauri imeigawa mitaa kwa mstari kuonyesha sehemu ambayo pikipiki ama gari linatakiwa kuegesha.

(c) Idadi ya magari yanayotakiwa kuegesha katika mtaa mmoja itaainishwa na Halmashauri au Wakala.

(d) Halmashauri au wakala anaweza kuainisha baadhi ya maeneo katika mitaa kuwa ni sehemu ya maegesho yaliyotengwa.

Kituo cha mabasi

5.-(1) (a) Hakuna basi litakaloruhusiwa kushusha,kupakia abiria wake katika eneo la Halmashauri zaidi ya maeneo yale ambayo yameanishwa kuwa ni vituo vya mabasi.

(b) Isipokuwa kwa kibali toka Halmashauri,mabasi yote yanatakiwa kuanzia safari zao katika vituo vya mabasi.

(c) Mabasi yanayofanya safari ndani ya Halmashauri hayaruhusiwi kukaa katika vituo vya njiani baada ya safari yake katika kituo cha basi kwa lengo la kushusha na kupakia abiria zaidi ya dakika tano.

(d) hairuhusiwi kwa basi kufanya matengenezo katika kituo cha basi.

(2) (a) kutakuwa na ada itakayolipwa kwa kila pikipiki ama gari litakalo egesha katika sehemu za kuegesha pikipiki ama magari kama itakavyoainishwa katika jedwali la Sheria hizi.

(b) ushuru wa kuegesha pikipiki na magari unaweza kulipwa kwa saa, kwa siku au mwezi.

(c) iwapo mtu atakuwa amelipia ada ya kuegesha kwa siku au kwa mwezi ataruhusiwa kuegesha gari ama pikipiki katika mtaa wowote ule kwa muda aliolipia bila ya kudaiwa tena

(d) ushuru huo utalipwa mara tu baada ya kuegesha gari ama pikipiki.

Maegesho yaliyotengwa

6.-(1) (a) Halmashauri au Wakala ataainisha maegesho yaliyotengwa baada ya kupokea maombi toka kwa mtu anayetaka kutengewa eneo la kuegesha magari na pikipiki.

(b) Baada ya maombi yake kukubaliwa na kulipia ada ya maegesho yaliyotengwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali katika Sheria ndogo hizi ataruhusiwa kutumia sehemu hiyo yeye peke yake bila ya kuingiliwa.

(c) Hata hivyo mtu ambaye amelipia ada ya maegesho yaliyotengwa atalazimika kulipia ada ya kuegesha gari iwapo atakuwa ameegesha nje ya sehemu iliyotengwa.

Muda wa kulipa Ada

7.-(1) Ushuru wa kuegesha gari ama pikipiki utatozwa kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kila siku.

(2) Ushuru wa maegesho utatozwa kwa kila saa moja ya maegesho na kwa kila muda unaozidi utatozwa tena kwa saa mpaka pikipiki ama gari litakapoondoka eneo la maegesho.

(3) kwa magari makubwa ambayo yatalazwa katika maeneo ya maegesho yatatozwa ushuru (overnight parking fees).

Kushindwa kulipa Ada

8. Mtu yeyote ambaye ni dereva au mmiliki wa gari ama pikipiki ambaye atakataa au kushindwa kulipa ushuru au kuegesha muda mrefu zaidi ya ule aliolipia kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

Kuzuia kuegesha

9.-(1) Halmashauri inaweza kuzuia kuegesha katika sehemu kwa kuweka alama au kibao kilichoandikwa "*Hakuna kuegesha hapa*" au "*No parking* "kwa sababu zifuatazo;

(a) kwa ajili ya kurahisisha mzunguko wa magari au kwa sababu za kiusalama.
(b) iwapo katika sehemu hiyo kuna ujenzi au ubomoaji unafanyika.
(c) au sababu yoyote ile ambayo inafanyika katika mtaa huo.
(d) magari ya mizigo na yasiyo ya mizigo hayaruhusiwi kufanyiwa matengenezo katika barabara za mitaa ndani ya Halmashauri isipokuwa katika gereji tu
(e) hairuhusiwi kuegesha au kulaza gari ama pikipiki kwenye barabara za mitaa zilizopo katika Halmashauri.

Kutoa taarifa

10.-(1) Mtu yeyote,dereva au mmiliki wa gari ama pikipiki atatakiwa kutoa taarifa kuhusiana na gari yake iwapo atatakiwa kufanya hivyo na Halmashauri au wakala.

(2) Mtu yeyote atakaeshindwa kutoa taarifa kuhusiana pikipiki na gari lake chini ya aya (1) ya Sheria hii atakuwa ametenda kosa.

Msamaha

11.-(1) Pikipiki na magari yafuatayo yamesamehewa kulipa ada ya uegeshaji chini ya Sheria hizi;

(a) magari yote ya wanadiplomasia
(b) magari na pikipiki za wagonjwa

(c) magari napikipiki za serikali
(d) magari na pikipiki zote za jeshi
(e) magari na pikipiki za zimamoto
(f) pikipiki ama gari ambalo linamshusha mtu ili mradi lisikae zaidi ya dakika tano.

(g) magari yote yanayofanya usafi katika eneo la Halmashauri
(h) Pikipiki na magari yote yaliyoegeshwa katika sehemu za kuabudia wakati wa ibada.

(2) Bila kuathiri kifungu cha (1) Halmashauri inaweza kusamehe gari au pikipiki yoyote ile kulipa ada ya kuegesha iwapo itaridhika na sababu alizotoa mwombaji wa msamaha huo.Msamaha huu utatolewa na kamati ya Fedha na Uongozi.

Makosa na Adhabu

12.-(1) Itakuwa ni makosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

a) atakayeegesha gari bila kulipia
b) atakaye egesha gari au pikipiki nje ya mstari uliochorwa kuainisha eneo la kuegesha
c) atakaye osha gari au pikipiki katika sehemu za kuegesha gari au pikipiki
d) atakaye egesha gari au pikipiki katika sehemu ambazo hazijaruhusiwa kuegesha gari.
e) kumzuia kwa namna yoyote ile Afisa Muidhiniwa kukusanya ushuru.
f) kushawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu chochote cha Sheria hizi Ndogo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi mitatu jela au vyote kwa pamoja yani faini na kifungo.

(3) Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kufifilisha kosa iwapo mkosaji atakiri kosa na kukubali kulipa faini.

JEDWALI LA KWANZA

USHURU WA KUEGESHA GARI

(Limetungwa chini ya kifungu cha 6(1),b cha Sheria Ndogo hizi)

SAFU YA KWANZA	**SAFU YA PILI**	
Aina ya gari	***Kwa saa***	***Kulaza gari***
Gari ndogo (Bajaji)	300.00	1,000.00
Pick up/Station wagon	500.00	1,500.00
Pikipiki ya magurudumu mawili	200.00	500.00
Malori ya mchanga		2,000.00